**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Mbeya**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu ya shule: 0748 066249**

**Mkuu wa Shule Na. 0755 186599**

**Makamu Mkuu wa Shule Na. 0754 806817**

**Matron Na. 0754 741179**

**Shule ya Sekondari NTABA**

**S.L.P 278 TUKUYU**

**Tarehe 11/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NTABA, HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO MKOA MBEYA MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya **HKL**.

Shule ya Sekondari Ntaba ipo katika kata ya **Kambasegela,** umbali wa Kilometa 29 Kusini mwa Mji wa **Tukuyu.** Usafiri wa moja kwa moja wa basi (costa) kutoka mjini **Mbeya** unapatikana katika kituo cha mabasi **Nane-nane** Nauli ni Shilingi 9,000/=
Au panda gari za **Tukuyu**, ukifika Tukuyu mjini usafiri wa **NTABA** unapatikana jirani na kituo cha mabasi kiitwacho **UWANJANI** kwa nauli Tshs: 5000/= mpaka **NTABA**.

Usafiri unapatikana kuanzia saa 4 asubuhi hadi saa 12 jioni. Shule ipo ndani ya mita 400 kutoka kwenye kibao cha shule(upande wa kulia ukitokea Tukuyu).

Wanafunzi wanaotokea **Kyela**, wapande gari za **Ipinda** nauli Tshs: 1500/= mpaka Ipinda, Ipinda mpaka Ntaba sekondari usafiri ni pikipiki nauli Tshs: 4000/=. Shule ipo upande wa kushoto ukitokea Ipinda.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14.08.2023** hivyo Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.08.2023**.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Sketi mbili ndefu zinazogusa soksi zenye rinda boksi kubwa mbili ,mbele na nyuma,pembeni rinda ndogo nne kila upande. Sketi moja blue bahari na nyingine nyeusi.

ii. Shati mbili mikono mirefu. Shati moja light blue na shati ya pili iwe nyeupe.

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) kwa Waislamu ni nyeupe moja na light blue moja sawa sawa na rangi ya shati za shule. Hijabu ziifunike kifua cha mwanafunzi pia ziwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama na vikofia vya kuvalia vyenye rangi hiyo hiyo;

iv. Tai mbili zenye rangi sawa na sketi ya shule. Tai moja blue bahari na nyinginge nyeusi.

v. Traksuti moja dark-blue yenye ufito mweupe.

vi. Sare ya Michezo ni jezi( tisheti na kaptula) rangi ya blue(kama Chelsea) na raba rangi yeyote (jozi moja);

vii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

viii. Nguo za kushindia (Shamba dress) rangi ya pink mtindo/mshono wa soro (kitambaa cha coshibo). Jozi moja.

ix. Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi.

x. Sweta la kijani iliyoiva (kijani kijeshi), mshono wa kawaida usio na urembo. Jozi moja;

xi. Tisheti (T-shirt) (zinapatikana jirani na shuleni kwa gharama ya Tsh: 10,000/= Jozimojo;)

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Daftari makubwa (counter books quire 4) ziwe 7, na qiure 2 ziwe 3. Jumla 10;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka. (Lazima ziletwe);
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Godoro moja, urefu futi 6, upana futi mbili na nusu;
*v.* Mashuka Jozi 2 (shuka moja rangi ya blue na shuka nyingine rangi ya pink), blanket nyepesi 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1*;*
vi. Fulana za ndani (vest) ziwe nyeupe 3 na nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, mopper 1, mifagio 2 wa ndani (soft brush 1) na wa nje (hard brush 1).
x. Sanduku (tracker) la kuhifadhia nduo.

### 2.3 Michango mbalimbali

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Ukarabati | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: Mwanafunzi asiye na bima ya afya(NHIF) anatakiwa kuja na fedha mkononi Tsh 7,000/= kwa ajili ya bima (CHIF) iliyoboreshwa**

Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule **NTABA SECONDARY SCHOOL Na.61403500067 NMB Tawi lolote lile (mahali popote). Mwanafunzi aje na (BANK PAY INSLIP).**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NB.***Unaweza kununua baadhi ya vitabu vya kujisomea vilivyoorodheshwa hapa chini***

**ENGLISH LANGUAGE**

a) James J. (2012, Advanced English Language, form six and form five, Oxford university press.
b) Asheri N. (2010) Advanced level English Second Edition, Good book publisher, Dar-es-salaam.

**ADVANCED LITERATURE**
**NOVALS**

c) A man of the people – Chinua Achebe
d) The Rape of the pearl – Magala Nyajo

**PLAYS**

e) A enemy of the people – Henrick Ibsen
f) The bride – Austin Bukenya

**POETRY**

g) Selected Poems – Institute of Education
h) The wonderful surgeon and other poems – Charles Mloka.

**VITABU VYA KISWAHILI**
**KSWAHILI. II**

a) JPD Company (2008) Kiswahili II kidato cha 5 & 6 General supplies Ltd Dar es salaam.

b) J.A. Masebo (2011) Nadharia ya fasihi kidato cha 5 na 6 Nyambari nyangwine publishers.

**USHAIRI**

c) Kimbunga – Haji Gora
d) Fungate ya Uhuru – Mohammad S. Khatibu
e) Mapenzi bora – Shaban Robert
f) Chungu tamu – T. Mvungi

**RIWAYA**

g) Mfadhili – Hussein Tuwa
h) Kufikirika – Shabani Robert
i) Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile
j) Vuta n'kuvute – Shafi A. Shafi

**TAMTHILIYA**

k) Morani **–** Emmanuel Mbogo
l) Kivuli kinaishi – Said Mohamed
m) Nguzo mama – Penina Mhando
n) Kwenye ukingo wa thim

**KSWAHILI. I**

o) Saluhaya (2010) Nadharia ya lugha STC DSM – Tanzania
p) Masebo J.A (2012) Nadharia ya Kiswahili kidato cha 5 na 6

**GENERAL STUDIES**

**a)** Nyambari Nyangwine (2009) Advance Level General Studies notes. Nyambari Nyangwine publishers

**HISTORY I & II**

a) Saleh Yassin. Essential in Advanced Level History Paper 1. Ahmadiyya Printing Press
b) Saleh Yssin. Essentials in Advanced Level History Paper 2. Ahmadiyya Printing Press
c) Shibitali C.K. Contemporary Historical Event. A-level History 1. Che Guevara Investment.
d) Shibitali C.K. Contemporary Historical Event. A-level History 2. Che Guevara Investment.
f) Oxford (2011) Advanced learners. History form 5 and 6. Oxford university press (T) Ltd. Dar-es-salaam.
g) Zisti Kamili (2015) Advanced level. History part one alive. Kot Dublishers.
h) Zisti Kamili (2015) Advanced level. History part two alive. Kot Dublishers
i) Walter Rodney, (1976) How Europe Underdeveloped Africa. TPH, DSM
j) Perry Davis, (1985) History of the world Houghton Milton Company Washington.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
    i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
    ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
    iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
    iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**MOTTO WA SHULE**: "**DARE TO FIGHT DARE TO WIN"**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NTABA**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule Na. 0755 186599**
- **Makamu Mkuu wa Shule Na. 0754 806817**
- **Mwandamizi Taaluma Na. 0768 333167**
- **Mwandamizi Malezi Na. 0757 075217**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**(The student should be examined by Government health centre)**

**NTABA SECONDARY SCHOOL,**

**P.O.BOX 278,**

**TUKUYU.**

**JULY,2023.**

**TO THE MEDICAL OFFICER,**

**MR/MRS** ……………………………………………………..………..……..

**STUDENT'S........................................................................................... (Full name)**

Please examine the above student to her/his physical and mental fitness for a full time student in this school.

The examination should have to involve the following categories.

1. Vision with glasses, right.................................left..........................................
2. Blood pressure…………….………………………………
3. haemoglobin…………………………..…………………………………………
3. F.V Bleeding ……………………………..…..………………………………..
4. Urine for sugar, Albumin and pregnancy ………………………………...……..
5. Stool for routine examination ……………………………...…………………
6. Venereal diseases ……………….……………...………………………………..
7. Neurosis ……………………………..………………………………………….
8. Any abnormality
   a) Heart …………………………………………….……………………
   b) Lung ……………………...…………………………………………...
   c) Speech ……………………..…………………………………………..
9. Are there any serious disease e.g. leprosy, epilepsy, Asthma, Diabetes ………….
   ………………………………………………………………………………………

**NAME OF MIDICAL HEALTH CENTRE** ………………………………..……………………..

**DOCTOR'S NAME AND SIGNATURE** ……………………………………………….……………

**Thank you,**

……………………………………….

**THE HEADMASTER,**

**NTABA SECONDARY SCHOOL.**

## VITAMBAA VYA SARE YA SHULE NA AINA YA MSHONO





## FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA TARATIBU ZA SHULE

**SEHEMU YA I**:( IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)
Mimi…..........................................................................................Nimezisoma sheria ,kanuni na taratibu za shule na kuzielewa vizuri bila ya shaka yoyote. Ninaahidi kuzitii na kutozivunja katika kipindi changu chote cha kusoma kwangu katika **shule ya sekondari Ntaba**. Sitashiriki katika mgomo wowote nikiwa shuleni. Vilevile, nitajitahidi kusoma kwa bidi na kushiriki shughuli zote za nje kulingana na ratiba ya shule. Endapo nitakwenda kinyume na kiapo cha ahadi yangu, basi uongozi wa shule unichukulie hatua za kinidhamu ikiwa ni Pamoja na kupewa **adhabu kali/kusimamishwa masomo na hata kufukuzwa shule.**

Dini ……………………………… Dhehebu........................................... Tarehe ya kuzaliwa………………...Michezo uipendayo/Hobbies ……………………………………..

Kazi ya mzazi/mlezi …………………………………………… mahali …………………... Wilaya……………………………………. Mkoa..........................................Simu ……………………. Jina la mwanafunzi ....................................................................Sahihi ……………………. Tarehe ………………

**SEHEMU YA II**: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI)
Mimi…...........................................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa Mwanafunzi...........................................................................kidato cha tano mwaka 2023; Ninakiri kuwa nimeyasoma maelekezo ya kujiunga na shule ya **Sekondari Ntaba** na kuyaelewa vizuri. Ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika kuhakikisha mwanangu anazingatia taratibu zote za shule wakati wa kipindi chote cha masomo yake. Pia, nitampatia mahitaji yake yote muhimu ya shule ikiwa ni Pamoja na malipo, mahitaji binafsi na kufuatilia mwenendo wake kitaaluma na nidhamu na niko tayari kupokea maamuzi yoyote yatakayotolewa na uongozi wa shule endapo mwanangu atavunja taratibu, kanuni na sheria za shule. Mwisho, endapo nitashindwa kutimiza jukumu langu la kumlipia mwanangu michango halali ya shule kwa wakati, niko tayari kuwajibishwa ikiwa ni Pamoja na kufikishwa katika vyombo vya kisheria kwani kufanya hivyo ni kuzorotesha maendeleo ya mwanangu na mipango ya shule kwa ujumla.

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………… Sahihi............Tarehe……….........

**SEHEMU YA III**: UHUSIANO WA MWANAFUNZI NA NDUGU/JAMAA WENGINE.

| Na. | **JINA LA NDUGU** | **PICHA** | **UHUSIANO** | **Na. YA SIMU** | **ANAKOISHI** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NTABA.**

**......................................................**

**MASTERFEL T. MWASHINDI**

**MKUU WA SHULE.**

**Na. 0755 186599.**